

»SATG magonjwa, wadudu na magugu kwa kilimo cha nyanya«

Nyanya ni mboga yenye lishe ya vitamini, wingi na ubora wake unadhamiriwa na aina na kiwango cha teknolojia inayotumiwa

Kupanda nyanya za kikaboni hupunguza hatari za kiafya na ina ladha nzuri. Mchakato na maandalizi ya kulima ni kuangazia hali ya hewa, utayarishaji wa ardhi, upandaji, umwagiliaji, kupogoa na kuvuna. Nyanya zinahitaji mwanga wa juu zaidi wa nyuzi 20–27 kwa kuota.

Usimamizi wa nyanya

Nyanya hukua vizuri kwenye udongo wenye uwezo wa kutoa na kunfyonza maji ifaayo hasa kwenye mchanga tifutifu wenye pH acidi na besi ya 6–7. Epuka ardhi iliyopandwa hapo awali nyanya, pilipili na mimea ya biringanya kwani ardhi hii inaweza kusababisha magonjwa na wadudu kuongezeka.

Andaa shamba wiki 2–3 kabla ya kupandikiza na weka mbolea mwezi mmoja kabla ya kupanda alafu tandaza na kuchanganya samadi ya wanyama na udongo. Tengeneza ardhi kwenye vitanda vyatupana wa mita 1 na urefu wa sentimita 30 ukiacha upana wa mita 1 kati ya vitanda na weka aina nyingi za mbolea katika msimu wa kupanda. Nyanya zinahitaji mbolea ya NPK, Magnesia, Kalisi, potashi. Panda mbegu katika trei za kuanzia na maji mara moja kwa siku kwa wiki 6–8 na udumishe joto la nyuzi 20–27 sentigredi kwa ajili ya kuota vizuri kwa mbegu. Baada ya kuota, ng'oa miche taratibu kutoka kwenye trei na upandikize kwa umbali wa sentimita 50 katikati ya mimea.

Maandalizi

Tandaza mimea kwa kutumia matandazo ya kikaboni kama vile vipandikizi vyatupana ya nyasi, majani, vumbi la mbao ili kuhifadhi unyevu na kutoa chakula kwa viumbe vidogo kwenye udongo na

kisha kushirikisha mimea inayokua ili kutoa msaada kwa mimea kukua kwenda juu. Nyanya mpya zilizopandikizwa zinahitaji kumwagiliwa maji kila siku kwa wiki 1–2 na mara moja kwa siku 10 hadi tone livunwe. Kata matawi yaliyokufa kwenye shina ili kuzuia kuchelewa kukomaa kwa mimea ili kuboresha ukubwa wa matunda, mzunguko wa hewa, kupunguza magonjwa ya majani na kuruhusu ukomavu wa mapema.

Hatimaye, vuna asubuhi kuzuia matunda kutoa mvuke au unyevunyevu mwangi na epuka uharibifu kwa matunda kwa utunzaji sahihi na usichanganye matunda yaliyoharibika na matunda ambayo hayajaharibika.